

*Huduma ya  
Kikristo ya  
Tony Alamo*

*Jarida la Dunia*



**Yerusalemu Mpya**

*Mchungaji Tony Alamo*

**Makanisa Ulimwenguni Kote**

*Taifa la Kikristo la Alamo*

**Tony Alamo Christian Church**  
NEW JERUSALEM MINISTRIES  
Services Every Evening 8pm - Sunday 3-6pm

**Toleo 17400**

# **JESHI NA JESHI LA ANGA LA MUNGU**

## **(WALINZI)**

**na Tony Alamo**



*Wachungaji Tony na Susan Alamo katika kipindi chao cha  
televisheni ya kimataifa picha ilichukuliwa mwaka wa 1973*

Mtumishi wa Elisha ali-kuwa ameamka mapema, ak-aona jeshi la Shamu lilikuwa limeuzingira mji ambao yeye na Elisha walikuwamo. Kwa hofu, akamwambia Elisha, "Ole wetu, Bwana wangu! Tufanyeje? [kwa maneno mengine, tutawezaje kutoka katika hali hii tukiwa hai? Ki-sha Elisha akamwambia mtumishi wake], Usiogope: kwa maana walio pamoja nasi ni wengi kuliko wale walio pamoja nao. Elisha Akaomba [kwa MUNGU] akasema, BWANA, NAKUSIHI, mfumbue macho yake, apate kuona. Na BWANA akayafumba macho ya mtumishi yule; naye akaona: Na, tazama, kile kilima kilikuwa kimejaa farasi na magari ya moto yaliyomzunguka Elisha pande zote" (2 Wafalme 6:15-17).

Jeshi lile lile au majeshi ya MUNGU ambayo Elisha alimwombwa Mungu amonyeshe mtumishi wake (mtumishi wa Elisha) ndilo jeshi lile lile ambalo MUNGU alitumia kuziangusha kuta za Yeriko (Yoshua 6:20). Yoshua alikutana na MKUU wa majeshi ya BWANA kule Yeriko katika njia hii : "Ikawa hapo, Yoshua alipokuwa karibu na mji wa Yeriko, akai-nua macho yake na kuangalia, na, tazama, mtu mwanamume akasimama kumkabili mbele yake, naye alikuwa na upanga wa

wazi mkononi MWAKE; Yoshua AKA-MWENDEA na KUMWAMBIA, Je! WEWE u upande wetu, au upande wa adui zetu? Naye akasema, LA; LAKINI NIMEKUJA SASA KAMA AMIRI WA MAJESHI YA BWANA [YESU kabla hajachukua mwili wa binadamu]. Naye Yoshua akaanguka kifudifudi mbele zake hadi chini, na kuabudu, na AKAMWAMBIA, BWANA wangu anamwambia nini mtumishi WAKE? Na AMIRI wa majeshi ya BWANA akamwambia Yoshua, Vua viatu vyako kutoka miguuni mwako; kwa kuwa mahali usimamapo ni Patakatifu. Na Yoshua akafanya vivyo.

"Basi mji wa Yeriko ulikuwa umefungwa kwa sababu ya wana wa Israeli: hapana mtu aliyetoka, wala hapana mtu aliyein-

gia. [Hii ilikuwa kwa sababu walijua kuwa MUNGU ali-kuwa pamoja na Israeli, na pia walijua kuwa MUNGU alikuwa anakwenda ku-waangamiza.] BWANA aka-mwambia Yoshua, Tazama, nimeutia Yeriko katika mko-no wako, na mfalme wake, na mashujaa wake.

"Nanyi mtawzunguka mji huu, watu wote wa vita, mki-uzunguka mji mara moja. Mtafanya hivi siku sita. [Hii ilikuwa ili kuwatia hofu watu wenyewe dhambi wa Yeriko

kabla ya maangamizo yao makamilifu] Na makuhani saba watachukua tarumbeta saba za pembe za kondoo waume, mbele ya hilo sanduku (la agano); na siku ya saba mtawzunguka mji mara saba, nao makuhani watapiga tarumbeta zao. Ki-sha, itakuwa watakapopiga hizo pembe za kondoo waume kwa nguvu, nanyi mtakaposikia sauti ya tarumbeta, watu wote watapiga kelele kwa sauti kuu; na ukuta wa mji utaanguka chini pale pale, [kazi hii itafanywa kwa mkono usioonekana wa BWANA wa majeshi], na hao watu (Waisraeli) watapanda, kila mtu akiendelea mbele kukabili.

"Basi Yoshua, mwana wa Nuni, akawaita makuhani, akawaambia, Lichu-

*(Inaendelea ukurasa wa 2)*

## JESHI NA JESHI LA ANGA LA MUNGU (WALINZI)

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)

kueni sanduku la agano, tena makuhani saba na wachukue tarumbeta saba za pembe za kondoo waume mbele ya sanduku la BWANA. Naye akawaambia watu, Piteni mbele, mkauzunguke mji, na hao watu wenye silaha na watangulie mbele ya sanduku la BWANA. Basi ikawa, Joshua alipokwisha kusema na watu, wale makuhani saba, [Wayahudi] wenye kuzichukua tarumbeta saba za pembe za kondoo waume walipita mbele za BWANA, wata-tangulia, wakazipiga hizo tarumbeta; nalo sanduku la agano la BWANA likiifuata. Na wale watu wenye silaha walikwenda mbele ya hao makuhani waliozipiga tarumbeta, na majeshi waliobakia wakafuata sanduku la agano, huku makuhani wakitembea na kuzipiga tarumbeta. Joshua akawaamuru watu, akisema, Msipige kelele, wala sauti zenu zisisikiwe, wala neno lolote lisitoke kinywani mwenu, hata siku ile nitakapowaamuru kupiga kelele, ndipo mtakapopiga kelele.

“Basi akalipeleka sanduku la BWANA liuzunguke huo mji, likauzunguka mara moja: Kisha wakaenda kambini wakakaa kambini. Joshua akaondoka asubuhi na mapema, nao makuhani wakalichukua sanduku la BWANA. Na wale Makuhani saba wakazichukua tarumbeta saba za pembe za kondoo wa kiume mbele ya sanduku la BWANA, wakaendelea wakizipiga tarumbeta; na Watu wenye silaha wakawatangulia, na hao waliokuwa nyuma wakalifuata sanduku la BWANA; makuhani wakizipiga tarumbeta wali-pokuwa wakienda. Siku ya pili wakazunguka mji mara moja, wakarejea kambini; ndivyo walivyofanya siku sita.

“Ikawa siku ya saba, wakaondoka asubuhi na mapema wakati wa mapambazuko, wakauzunguka mji vivyo hivyo mara saba; ila siku hiyo waliuzunguka huo mji mara saba. Ikawa mara ya saba, makuhani walipozipiga tarumbeta, Joshua akawaambia watu, Pigeni kelele; kwa maana BWANA amewapeni mji huu. Na mji huu utakuwa wakfu kwa

BWANA, mji wenyewe na vitu vyote vili-vyomo; Isipokuwa Rahabu yule kahaba, ataishi, yeze na watu wote walio pamoja naye nyumbani, kwa sababu aliwaficha hao wapelelezi tuliovatuma. Na ninyi msikose kujiepusha na kitu kilichowekwa wakfu; msije mkakitwaa kitu kili-chowekwa wakfu, baada ya kukiweka wakfu; nanyi hivyo mtayafanya matukio ya Israeli kuwa yamelaaniwa na kufadhaisha. Lakini fedha yote, na dhahabu, na vyombo vya shaba na chuma ni vita-katifu kwa BWANA; vitaletwa katika ha-zina ya BWANA.

“Basi watu wakapiga kelele, na makuhani wakazipiga tarumbeta; hapo, watu waliposikia sauti ya tarumbeta, hao watu wakapiga kelele kwa sauti kuu sana, na ule ukuta wa mji ukaanguka nchi (chini) kabisa [jambo hili lilifanikishwa na majeshi ya BWANA na MKUU wa majeshi ya BWANA], hata watu wakapanda juu, wakaingia katika mji, kila mtu akiendelea kukabili mbele; wakaut-waa huo mji” (Joshua 5:13-6:20).

Katika kitabu cha Enoki, Nabii mkuu Enoki anatabiri kuhusu walinzi. Hawa walinzi ni malaika wa MUNGU, na ni jeshi la mbinguni la BWANA. Wakati mwininge wanasemekana kuwa malaika walinzi wa watakatifu wa MUNGU hapa duniani.

Kunao malaika wabaya, na kuna malaika wazuri. Ufunuo 12:4 inasema kwamba theluthi moja ya malaika hawa – wale wabaya – walitupwa kutoka Mb-inguni pamoja na kiongozi wao, Shetani mwenyewe (Luka 10:18). Lakini kumbuka, theluthi mbili ya malaika – wale wazuri – walibakia kwenye utumishi wa MUNGU. Wale wabaya, theluthi moja, si wabaya tu, bali ni hatari sana

Ufunuo 12:3 inasema “IKAONEKA-NA ishara nydingine mbinguni; Na taza-ma, joka kubwa jekundu [shetani], lili-kuwa na vichwa saba...” “Vichwa saba ni milima saba [ya Roma, Italia], ambapo mwanamke amekaa” (Ufunuo 17:9).

Mwanamke huyu ni nabii wa uongo, kanisa la uongo, kanisa la kishetani, kichwa cha yule mnyama ambaye ni Vatican, kanisa la katoliki la Kirumi, mashoga, kanisa linalo nyanyasa watoto kijinsia.

Ufunuo 12:3 inaendelea kusema kwamba hivi vichwa saba vina pembe

kumi. Hizi pembe kumi zinaashiria Mataifa kumi ya Ulaya ambayo yanaipa nguvu Vatican Roma (Umoja wa Mataifa, Mpangilio Mpya wa Dunia) kwa muda mfupi (taifa la mwisho likiwa ni Ugiriki), ambayo yamejiunga pamoja na Mpangilio Mpya wa Shetani, au serikali moja ya dunia. “...na vilemba (taji) saba kichwani mwake [hivi vilemba (taji) saba vinawakilisha mpangilio mpya wa dunia wa Shetani ambao kwa muda utatawala mabara yote saba, au kwa maneno, men-gine dunia nzima].”<sup>1</sup>

“Na mkia wake wakokota theluthi moja ya nyota za Mbinguni [Nyota ni malaika waovu].<sup>2</sup> Ufunuo 1:20 inasema nyota ni ishara ya malaika], na [joka, Shetani] aliwatupa [theluthi moja ya wale malaika waovu na wabaya] duniani: Na yule Joka [Shetani] akasimama mbele ya mwanamke yule [aliye na zile nyota kumi na mbili kwenye taji lake. Huyu (Mwanamke) ni Bibi Harusi wa KRISTO, Yerusalem Mpya, ambaye ni MWILI halisi wa KRISTO hapa duniani, Israeli wa kweli, wale walio Wakristo, siyo kamwe wakatoliki, waliotokana na watu wa Mungu waliochaguliwa, Wayahudi. Sasa MUNGU anatoa wokovu kwa watu wa mataifa yote ambao watampokea KRISTO kama wokovu wao” (Ufunuo 12:4).

Ufunuo 12:4 inasema mwanamke huyu (MWILI wa KRISTO) alikuwa kari-bu kuzaa mtoto, ambaye alikuwa KRISTO. Hii inaturudisha nyuma hadi wakati ule Shetani, kupitia kwa Mfalme Herode na jeshi lake, alikuwa amesimama mbele ya Israeli ili kumwangamiza KRISTO wakati wa kuzaliwa KWAKE na/ au miaka miwili iliyofuatia,<sup>3</sup> kwani KRISTO bado alikuwa MFALME wa wafalme na BWANA wa mabwana, MWOKOZI wa ulimwengu, YEYE ambaye angezihari-bu kazi za Shetani kwa kuokoa nafsi za wote ambao WANGEMKUBALI kama MWOKOZI na mamlaka yao.<sup>4</sup> Wakolosai 2:15 inasema kwamba KRISTO “ak-ishawapokonya nguvu na mamlaka yao hao pepo watawala... aliwafanya kuwa kitu cha fedheha hadharani, akawashinda katika msalaba.”

Hizi ni siku za mwisho.<sup>5</sup> Dunia imejawa na jeshi la MUNGU, na anga imejawa na jeshi la anga la MUNGU. Hizi

<sup>1</sup> Dan. 2:40, 7:19-25, Ufu. 13:2-8, 14:8, Kifungu 17, 18:2-24  
6:14-16, Ebr. 2:14-15, I Yoh. 3:8, 4:14-15, Ufu. 17:14, 19:16

<sup>2</sup> Isa. 14:12-17, Mat. 25:41, Lk.10:18, 2 Pet. 2:4, Yuda mstari 6, Ufu. 12:3-4, 7-9  
<sup>3</sup> Mat. 2:1-18    <sup>4</sup> Dan. 7:13-14, 1 Tim. 2:14-16, Ebr. 2:14-15, I Yoh. 3:8, 4:14-15, Ufu. 17:14, 19:16  
<sup>5</sup> Mat. Sura ya. 24

ni UFOs ambazo mamilioni ya watu wameziona ulimwenguni kote. Kwa sababu watu wa ulimwengu hawalijui NENO la MUNGU, wanaamini kuwa viumbe hawa (UFOs) ni wageni kutoka kwenye sayari zingine. Tukifahamu Biblia, tunafahamu jinsi gani watu wa ulimwengu wamedanganyika, kwa sababu hivi “visahani vinavyoolea angani” (viumbe vilivyo na umbo la sahani vinavyoolea angani) vinavyoitwa UFOs, havitoki kwenye sayari nyingine. Hawa ni “walinzi,” malaika wa MUNGU, wanaoichunguza kwa undani dunia kabla ya KRISTO kurudi duniani tena. Walinzi wanajitarishia hukumu.

Ufunuo 16:1 inasema, “Kisha nikasikia sauti kuu kutoka Hekaluni, ikiwaambia wale malaika saba, enendeni mkavimimine vile vitasa saba vya ghadhabu ya MUNGU juu ya nchi.” Katika Danieli 4:13, “Mlinzi [malaika] na mtakatifu walishuka kutoka mbinguni” Wakileta hukumu ya MUNGU kwa mfalme aliyejewa na kiburi Nebukadreza, aliyesema kwenye kitabu cha Danieli 4:30, “Mji huu sio Babeli kubwa nilioujenga mimi, uwe kao langu la kifalme, kwa uwezo wa nguvu zangu [badala ya nguvu za MUNGU], ili uwe utukufu wa enzi yangu [badala ya utukufu wa MUNGU]?”

Hii hapa ni hukumu ambayo MUNGU alimpa mlinzi ili kuifanya dhidi ya Mfalme Nebukadreza: “Hata neno lile lilipokuwa [bado] katika kinywa cha mfalme [aliyejawa na kiburi] sauti ilikuja kutoka mbinguni, ikisema, Ee Mfalme Nebukadreza, maneno haya unaambiwa wewe; Ufalme umeondoka kwako. Nawe

utafukuzwa [na walinzi] mbali na wanadamu, na makao yako yatakuwa pamoja na wanyama wa kondeni ; uthishwa majani kama ng’ombe, na nyakati saba zitapita juu yako, hata utakapoju ya kuwa yeye ALIYE JUU SANA ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa AMTAKAYE ye yote. Saa iyo hiyo jambo hilo likitimizwa, likampata Nebukadreza: Alifukuzwa mbali na wanadamu, akala majani kama ng’ombe, na mwili wake ulilowa maji kwa umande wa mbinguni, hata nywele zake zikawa kama manyoya ya tai, na kucha zake kama kucha za ndege” (Danieli 4: 31- 33).

Katika kitabu cha Yeremia 4:16, MUNGU alimwambia Yeremia, “Wapasheni mataifa habari; angalieni, hubirini juu ya Yerusalem, ya kwamba walinzi wanatoka nchi ya mbali, wanatoa sauti yao juu ya miji ya Yuda.” Kumekuwa na ghadhabu kubwa dhidi ya miji ya Yuda. Hii ni kwa sababu bado wanamkataa YESU kama MASIHI hadi leo hii.

Ninaamini kwamba karibu kila mtu duniani anafahamu kuhusu mamilioni ya kuonekana kwa UFOs (vitu vipaavyo angani visivyojulikana), lakini sio UFOs. Ni walinzi au malaika wa MUNGU wanaoipeleleza dunia katika hizi siku za mwisho kabla tu ya hukumu ya MUNGU, mwisho wa dunia, mwisho wa wakati. Katika huruma za MUNGU, ANAKUBALISHA kila mtu kushuhudia mamia ya nabii za siku za mwisho, ishara, na maajabu kama vile walinzi, malaika wa MUNGU, wanaoipeleleza dunia kwenye vinavyosemekana kuwa “visosa vinavyopaa angani”

kabla tu haijaangamizwa (dunia). Kitabu cha Yoeli kinatoa unabii huu,<sup>6</sup> kama vile afanyakyo mtume Petro katika kitabu cha Matendo ya Mitume: “Itakuwa siku za mwisho, asema MUNGU, nitawamwagia watu wote ROHO YANGU na wana wenu na binti zenu watatabiri, na wana wenu wataona maono, na wazee wenu wataota ndoto: Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake ROHO YANGU; nao watatabiri: Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu, na ishara katika nchi chini; damu na moto, na mvuke wa moshi: Jua litageuka kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla ya kuja kwa ile siku ya BWANA iliyo kuu na iliyo dha-hiri: Na itakuwa, kila atakayeliitia jina la BWANA ataokolewa” (Matendo 2:17- 21).

Walinzi, amba ni malaika wa Mbunguni, na sisi tulio Wakristo (siyo wakatoliki), tuna uhusiano kwa kuwa MUNGU alituumba sote. MUNGU aliumba malaika, na MUNGU alituumba sisi. Kuna wanadamu wema, na kuna wanadamu wabaya, kwa sababu ni wachache wetu tu amba tunazitimiza amri za MUNGU.<sup>7</sup> 1 Yohana 2:3-4 “Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua YEYE, ikiwa tunashika amri ZAKE. Yeye asemaye, nimemjua wala hazishiki amri zake, ni mwongo na kweli haimo ndani yake.”

Baadhi ya watu wanajivuna kuwa wanampenda BWANA. Hata hivyo, katika maisha yao ya kila siku, hawaiiwii wito wa MUNGU, badala yake huipuza sauti YAKE. Wengine wanasesma wanampenda BWANA wanapokua katika msisimko wa hisia. Kwa mfano, wanapojisikia kuangalia sinema, au kuangalia kipindi kwenye runinga, tukio la michezo, au tukio la muziki, kuna kitu ndani yao kinachowakataza kwenda, lakini wanenda hata hivyo. Wanajua kwamba hawapaswi kutenda dhambi kubwa, lakini hawajalishwi na yale wanayofikiria kuwa ni mambo madogo madogo. Wakati wanaposali kwenye ibada, wanaweza kutoa ushuhuda kuwa wameguswa na ROHO wa BWANA. Kuna watu wengi wanaojiita wakristo amba wako hivi. Kwa kweli, kumpenda BWANA kwa namna hii hakuna maana.<sup>8</sup>

Dada mmoja anawenza kuwa na ari  
(Inaendelea ukurasa wa 4)

<sup>6</sup> Yoe. 2:28-32    <sup>7</sup> Mat. 7:13-14, 21-23, Lk. 13:23-30  
<sup>8</sup> Mat. 7:21-23, Sura ya. 25

## Kutoka katika laini yetu ya maombi na habari ya masaa 24

Mchungaji Wilimena Thomas (wa Lauderdale, FL) alipokea kifurushi chake. Kina mama wote walio katika kikundi chao cha kusoma Biblia walikaa na kuanza kusoma “Jeshi na Jeshi la anga la MUNGU.” Alisema walijifunza mengi zaidi kutoka kwenye taarifa hii kuliko yote waliyowahi ku-jifunza kutoka kwa wachungaji wengine wote kwa miaka mingi (hawajapata kuwasikiliza hao wachungaji kwa muda sasa). Wote walifurahia nakala na wanazisikiliza kanda (CD). Walisema hakuna mtu anayeweza kuchambua na kuelezea mambo kama Tony. Alisema “tafadhalii naomba muendelee kuitumia nakala na kanda (CD)”. Wanataka tujue ya kwamba hao hujumui-ka na kuwa na mikutano ya maombi, na kwamba wanamwombea Tony na kanisa lote. Aliomba tena aweze kutumiwa jarida na kanda. Pia aliliomba kanisa kuwaombea wajukuu wake watatu waliopotea amba wamekuwa wakihubiriwa kwa miaka mingi.

## JESHI NA JESHI LA ANGA LA MUNGU (WALINZI)

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 3)

kubwa juu ya BWANA kwamba kaka kumi kwa pamoja hawawezi kumfikia. Anapoongelea kuhusu kumpenda BWANA, wanaomsikiliza wanaweza kuguswa kiasi cha kutokwa na machozi. Cha kushangaza hata hivyo, yule dada anapokuwa na hasira, hakuna anayeweza kumshika. Maisha kawaida ni maisha yasiyo ya uhalisia (maisha ambayo si ya MUNGU). Siku moja, yote yaliyo ya maisha ya kawaida lazima yavunjwe vipande vipande. Tunahitaji kuguswa kweli na BWANA kuona vizuri shauku yetu, bidii yetu ya uongo, mapenzi yetu ya uongo kwa BWANA, na utumishi wetu wa uongo kwa BWANA yote ni ya kawaida na haina hata chembe ya MUNGU ndani yake, si ya kweli. Hailjalihi kiasi cha safu za kuta za chuma shaba, ambazo tuko nazo, na hajjalishi hata lile lango la nje, lango la kati, au lango la ndani, haya yote ni lazima yafunguliwe moja baada ya jingine, kwa BWANA, kulingana na ROHO aliye ndani. Kisha tutatambua kwamba katika maneno yetu ya shauku na bidii, hatuwezi kumwona BWANA MWENYEWE. Ila tu wakati tumeon-gozwa au kuguswa na BWANA kiasi cha kwamba YEYE anaweza kuachiliwa kwa ukweli kutoka ndani mwetu hapo ndipo

tutaweza kuzaa matunda mengi, kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Yohana 15:2. Tunda lililo kwenye mti linapati-kana kwa sababu ya UHAI uliomo.

Hivyo basi, wanadamu wenyewe uhustiano na malaika waovu ni wanadamu waovu. Lakini kumbuka, kuna malaika wengi wa MUNGU kuliko malaika waovu. Elisha alimwonyesha mjakazi wake haya wakati jeshi la Shamu lilipowazunguka. Elisha alimsihi BWANA kufunga macho ya mtumishi wake ili aweze kuona kuwa kulikuwa na wengi pamoja naye na pamoja na Elisha kuliko walikuwa na Washamu. Wakati aliyatenda, "Tazama, kile kilima kilikuwa kime-jaa farasi na magari ya moto [majeshi ya BWANA] yaliyomzunguka Elisha [na mtumishi wake]," Jinsi majeshi ya ufalme wa MUNGU yalivyo leo pamoja na walinzi wakituzunguka na kutulinda, wakiyaangalia yote ambayo kila mmoja anasema na kutenda hapa duniani (2 Wafalme 6:17). Haya yanatokea kupitia kwa walinzi wa MUNGU kila mahali katika mbingu kwa visahani vinavyoelea angani na kwa walinzi duniani - jeshi la ardhini na jeshi la angani la MUNGU.<sup>9</sup>

Ni wakati muafaka kwa kila mtu ulimwenguni kutubu dhambi zake na kumtafuta MUNGU kwa moyo wote, roho, akili na nguvu zote, ambayo ndio amri ya kwanza na yenye umuhimu kuliko zote.<sup>10</sup> Hivi punde anga ya mashariki itajaa ishara ya MWANA wa ADAMU. Kuna maandiko

<sup>9</sup> 2 Nya. 16:9, Zek. 1:7-11, 4:10, 6:1-7, Ufu. 7:1-3 <sup>10</sup> Kum. 4:29, 6:5, 10:12-13, 11:13-14, 13:3-4, 16, 20, 26:16, 30:6, Yos. 22:5, Mat. 22:37-40, Mk. 12:29-31, Lk. 10:27

## Kenya

Mpendwa Mchungaji Tony Alamo,

Salamu katika jina lenye nguvu lililo kuu kuliko majina yote, jina la Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Nina furaha kukuarifu kwamba tunauchukua mji wetu kwa kutumia nakala za Alamo mnazotusambazia. Tunamfikia kila mtu aliyeokoka na asiyeokoka, na kwa mwezi mmoja uliopita tumeshuhudia watu 15 wakiokolewa na wako Kanisani. Pia, tumepokea kifurushi ulichotuma tarehe 21 ya mwezi Desemba. Tunakushukuru huku tukiomba nakala zaidi na Biblia kwani kuna hitaji kubwa. Mungu akubariki, wakati tukiendelea kumwomba Mungu aingilie kesi ya Mchungaji wetu, kwa maana najua kupitia maombi mambo yote yanaweze-kana.

Wako katika Kazi ya Bwana, Mchungaji Dalmas Munoko

Bungoma, Kenya

kadhaa yanayofafanua tukio hili. Moja ni kutoka kitabu cha Mathayo sura ya ishirini na nne. Andiko lingine ni kutoka sura ya pili ya kitabu cha Isaya. Pia lingine liko katika kitabu cha Ufunuo sura ya sita.

Mathayo 24:30-51 inasema "Ndipo itakapoonekana ishara yake MWANA wa ADAMU mbinguni; ndipo mataifa mengi ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona MWANA wa ADAMU akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. NAYE atawatuma malaika ZAKE [jeshi la BWANA, walinzi] pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule WAKE kutoka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu. "Basi kwa mtini jifunzeni mfano huu; Tawi lake likiisha kuchipuka na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno u karibu; nanyi, mya-onapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, mlangoni. Amin nawaambia, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia. Naam, Mbingu na nchi zitapita; lakini MANENO YANGU

## Peru

(Imetafsiriwa kutoka Kihispaniola)

Mungu akubariki, Ndugu Tony Alamo na Huduma yako,

Nakujulisha kuwa kwa utukufu wa Mungu, sasa tuna kanisa jipya. Ni mwendo wa saa tatu kutoka Salluna, karibu na Piura, mahali paitwapo Sechura, ambapo tuko na ndugu watu wazima 23 na watoto 33. Tunataka kufanya kazi binafsi, kusambaza maandiko yako nyumba kwa nyumba na wengi walitaka kuendelea kufunzwa. Jana tulijumuika na wapendwa wengi walikuja. Walimkubali Bwana na tutakuwa tukikutana mara tatu kwa juma. Utukufu uwe kwa Bwana. Yesu anakuja upesi.

Andres Chiroque Silva

Tony Alamo Ministries  
Sullana, Peru



**HUDUMA ZA ALAMO MTANDAO NI**  
**www.alamoministries.com**

hayatapita kamwe...kwa maana kama ilivyokuwa siku za Nuhu, Ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake MWANA wa ADAMU. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika, watu waliokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile alipoingia Nuhu katika Safina, wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake MWANA wa ADAMU.. Kesheni basi: kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu. Lakini fahamuni neno hili: kuwa mwenye nyumba angalijua ile zamu mwivi atakayokuja, angalikesha, wala asingaliiacha nyumba yake kuvunjwa. Kwa sababu hiyo, ninyi nanyi jiwekekeni tayari: kwa kuwa katika saa msiyodhani MWANA wa ADAMU yuaja. "Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu na mwenye akili, ambaye bwana wake alimweka juu ya nyumba yake, awape chakula kwa wakati wake? Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo. Amin nawaambieni, atamweka juu ya vitu vyake vyote. Lakini mtumwa yule mbaya akisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia; Akaanza kuwapiga wajoli wake, na kula na kunywa pamoja na walevi; Bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani na saa asi-

yojua, Atamkata vipande viwili, na kumwekea fungu pamoja na wanafiki; Ndiko kutakuwa na kilio na kusaga meno."

BWANA hutupa ishara nyingi, hivyo basi, ukiwa makini, hautakutwa ukiwa haupo tayari. Hapa yako maono mengine ambayo unapaswa kuyaweka akili ni mwako, kwa sababu maono haya yanakwenda kuwa ukweli upesi kuliko udhaniavyo: "Kisha nikaziona mbingu zimefunuka [haya ni maono mengine ya mwisho wa wakati kutoka kwa MUNGU], na tazama farasi mweupe, NA YEYE aliyempanda, aitwaye MWAMINIFU na WA-KWELI, naye kwa haki AHUKUMU na kufanya vita. Na macho YAKE yalikuwa kama mwali wa moto, na juu ya kichwa CHAKE taji (vilemba) nyingi; naye ana jina lililoandikwa, asilolijua mtu ila YEYE MWENYEWE. NAYE amevikwa vazi lililochovywa katika damu: Na jina LAKE aitwa, NENO la MUNGU. NA MAJESHI YALIYO MBINGUNI WAKAMFUATA, WAMEPANDA FARASI WEUPE [huyu ni BWANA na jeshi LAKE, walinzi], na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe safi. Na Upanaga mkali hutoka kinywani MWAKE, ili awapige mataifa kwa huo: NAYE atawachunga kwa fimbo ya chuma, [NENO la MUNGU]: naye anakanyaga shini-

kizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya MUNGU MWENYEZI. NAYE ana jina limeandikwa katika vazi LAKE na paja LAKE , MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA [Huyu ni YESU BWANA wetu]" (Ufunuo 19:11-16).

Kwa sasa twaishi katika dakika za mwisho za nyakati za mwisho. Dalili zote ziko hapa. Serikali moja ya dunia ya mpinga Kristo inaendelea na operesheni yake sasa. Kitengo cha anga cha MUNGU kimekua katika operesheni kwa miaka mingi, na mamia ya mamilioni ya watu wamewaona (vijisahani vinyoolea angani, walinzi, malaika jeshi la anga la kifalme la MUNGU). Papa kule Roma anajivunia jinsi Mpango Mpya wa Dunia ulivyo wa ajabu. Kuna Sunami, dhoruba za bahari, mitetemeko ya ardhi, mapigo ya kila aina, magonjwa, mifarakano baina ya mataifa, mateso, na mamia ya laana za kila aina.

Lazima uwe mwema au mbaya.<sup>11</sup> Aidha, utampokea KRISTO kama MWOKOZI wako, au UTAMKATAA. MCHAGUE sasa, kabla hujachelewa. Umebakiza pumzi moja, pigo moja la

*(Inaendelea ukurasa wa 8)*

**11** Mat. 7:15-20, Yak. 3:11-12, Ufu. 20:11-15, 21:7-8, 24-27, 22:11-12, 14-15

## Ushuhuda wa Steven Wedel

Jina langu ni Steven Wedel. Nilitimiza miaka 59 mwishoni mwa Oktoba, 2012. Nilimpokea Kristo kama Mwokozi wangu mnamo Novemba 4, 1971. Nilikuwa tu ndio nimetimiza miaka 18 juma moja kabla. Kama Kristo asingeingia maishani mwangu wakati alifanya hivyo wakati huo, inawezekana mngesoma tangazo langu la tanzia miaka iliyopita, badala ya nafasi ya kusoma ushuhuda wa nguvu za Mungu na uwezo wa kubadilisha maisha ya mtu mnaosoma sasa.

Nilipohitimu elimu ya Shule ya sekondari majira ya kipupwe cha 1971, si-kuwa na tamaa ya kuendelea na elimu ya chuo. Nilikuwa mmoja wa kundi lililoitwa Pseudo-hipie. (hili ni kundi ambalo lilikuwa nchini Marekani miaka ya sitini. Washiriki waliasi kinyume cha serikali na jamii.) Niligonga barabara kwenda San Fransisco, mara ya kwanza ni-

kiwa na marafiki wengine kwenye gari, na baadaye kwa kuomba lifti kwa watu wenye magari waliokuwa barabarani kutoka San Fransisco kwenda Boulder, Colorado, kisha kurudi tena California, wakati huu sasa kwenda Los Angeles.

Mama wa rafiki yangu mmoja niliyekuwa nikisafiri naye alikuwa na nyumba kubwa nzuri katika Beverly Hills. Alitualika tukae naye kwa muda, hadi wakati tungepata kazi na chumba cha kuishi ili tuhamie mle. Nyumba yake ilikuwa na bwawa zuri la nje la kuogelea na mtumishi wa kike aliyefanya mambo yote ya ununuzi na kutupikia. Yalikuwa mazingira ya likizo ya kufurahisha lakini ulikuwa wakati wa huzuni nyingi sana maishani mwangu.

Nilihisi ndani yangu ni kama nilipotea kabisa na bila matumaini katika maisha yangu. Hakukuwa na kitu ambacho kingeweza kutoa kuchanganyikiwa kwa



*Ndugu Steven Wedel*

mara kwa mara akilini na rohoni mwangu kuhusu maana ya maisha na kusudi lake. Nilihisi kutekwa ndani. Nilitaka maisha yenye maana, ambayo yangeweza kuwasaidia wengine. Nilifadhaishwa na hali katika dunia iliyonizunguka, rushwa, kutojali , uhalifu na umwagaji damu. Nilitaka kuishi katika dunia ya amani na hapo awali nilidhani kuwa mwondoko wa hip-

*(Inaendelea ukurasa wa 6)*

## Ushuhuda wa Steven Wedel

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 5)

pie kule California ungeweza kunipa jibu mbadala kwa mfumo wa maisha ya mbio ulionizunguka pande zote. Nilidhani ku-vuta bangi na hashishi, kutumia LSD na madawa mengine ya kulevy yaletayo njozi yangenipa ufahamu niliokuwa ni-kiutamani, katika kupata sababu ya mai-sha niliyokuwa nikiishi. Mimi sikutaka kazi ya tangia asubuhi saa tatu hadi jioni saa kumi na moja, nyumba ilio na mbwa na paka, na siku za usoni ambazo hazina mwelekeo. Nilitaka kujua maisha yali-faa kuwa na sababu gani. Kile ambacho madawa ya kulevy yalinifanya ilikuwa kuniibia akili yoyote niliyokuwa nimebaki nayo na kuniacha na uwezo mdogo sana wa kufikiria na kufanya chochote kabisa. Nilifikiri ninarukwa na akili na bila shaka yoyote, pengine nilikuwa. Lakini sikuwa nimelelewa kwa njia hii kamwe.

Nilikulia ughaibuni. Baba yangu alifanya kazi na shirika la kimataifa la YMCA mjini Tokyo, Japan, na tulihudhuria kanisa kila Jumapili katika kanisa lisilo la dhehebu lolote. Nilifundishwa kwamba sisi ni wakristo, na kufundishwa kuwa na ubinadamu, na kuwasaidia wengine. Nili-jua kuwa Krisimasi na Pasaka zilikua ni siku maalumu, na kwamba siku hizi hazi-kuwa na uhusiano wowote na Santa claus au Easter bunny (Sungura). Niliamini katika nafsi yangu, kama watoto wen-gine kwamba yupo Muumbaji, Mungu aliyeumba kila kitu, ikijumulisha mimi mwenyewe. Nilifundishwa kumwamini Yesu Kristo kama mwokozi, na bado si-kuja Yesu alikuwa nani haswa. Sikuwa na nguvu maishani mwangu, sikuwa na nguvu ya kushinda dhambi, na kwa kweli, nikiangalia nyuma, kati ya makanisa nili-yowahi kushiriki hakuna hata moja lililonifundisha maana halisi ya dhambi. Siku-wahi sikia msemo "kuzaliwa mara ya pili kwa roho" na sikuwahi kushuhudia watu wakiitwa kuokolewa madhabahuni katika makanisa yote hayo. Yalikufa kiroho kama niliyokuwa mimi.

Nilikua nikielekea darasa la kumi wakati familia yetu ilirudi Marekani. Sikutaka kuendelea kuwa mfu kiroho. Watu wote walionizunguka walikuwa waasi katika ule mwondoko wa Hippie. Nilianza kwa bidii kutafuta majibu

ya maswali mengi ndani yangu kuhusu maisha, kifo, maisha ya milele, kusudi. Nilisoma vitabu vya dini za mashariki ya mbali, dini za mafumbo au kiajabu-ajabu, dini za Wahindi wazaliwa wa Marekani, falsafa, vitabu vya mawazo na maadili mbalimbali, vitabu vya kikomu-nisti, ujamaa, ubepari, na kila kitu kili-chonija akilini. Nilisoma Biblia, lakini kwa wakati huo, bila Roho wa Mungu ndani yangu, sikuweza kulelewa. Nili-fanya mkarara (maneno yanayorudiwa-rudiwa yafanywayo na watu wa dini to-fauti tofauti), Yoga, kutembea misituni, nikijaribu niwezavyo kutokosea, ili niwe karibu zaidi na Mungu. Hakuna kili-cheweza kujaza utupu uliokuwa ndani yangu. Hakuna kilicho fanya kazi.

Kwa wakati ule sikujua, ila ninajua sasa, kuwa ni Bwana aliyekuwa akiten-da kazi ndani yangu na kunileta mahali ambapo angeweza kukinyenyekenza ki-buri changu chenyе ukaidi ili nimpokee ye ye kama Bwana na Mwokozi wangu. Alikubali kwamba hiari zote nilizokuwa nazo zididimie. Labda hakuhitaji ku-

fanya haya kwako, lakini alijua kwamba hii ndiyo njia pekee ambayo ingefanya machaguo mengine yote yapote. Kwako anaweza akafanya tofauti na kwangu, la-kini alijua kuwa ile ndio ilikua namna pekee ya kunifanya nijirudie. Alikuwa amenikubalisha kuja California ili ani-lete kwenye kusudi hili. Alikuwa aki-fanya kazi kwangu, lakini sikuyafahamu hayo wakati huo.

Katika Hollywood, California hun-geweza kutembea futi 200 kule Holly-wood Blvd bila kukutana na washuuda kutoka kwenye taasisi ya Tony na Susan Alamo. Walikuwa kila mahali ambapo ulienda. Wakati wowote nilipokuwa Hollywood, katika hali ya kutafuta ajira au kupitisha muda, walikuwa kila mahali wakipeana nakala za injili na kuwakaribishwa watu kwenye ibada kanisani mwao. Walijaa bidii ya Mungu. Nilishuhudiwa



*Ndugu na dada wa Huduma ya Alamo wakihudumu kwenye makazi ya kutunza wazee.*

kuhusu Mungu mara kadhaa na kukaribishwa kanisani kama wengine wengi, lakini nikakataa makaribisho yale tena na tena. Nilikuwa bado nimejaa njia zangu binafsi hivi kwamba singewenza kuwasikiliza wengine wakiniambia kuhusu Yesu. Wakati mwingi ingawaje, katika ule unyamavu wa usiku, wakati misukosuko ya siku ilikuwa imekwisha nami nikajipata peke yangu, Bwana angeanza kuyaleta mambo ambayo hawa wakristo walikuwa wameniambia kwa mawazo yangu, maandiko matakatifu ambayo walikuwa wamenionyesha kwenye Biblia kuhusu siku za mwisho, mambo ambayo yalionekana kwa urahisi kila mahali, maandiko kuhusu maisha ya milele na Jehanamu ambayo yalinifanya nishangae. Kutoka nje, Shetani alikuwa angali akinivuta huku na huko, lakini ndani Mungu alikuwa akinivunjavunja.

Siku moja mchana, Mungu alimaliza yale aliyokuwa ameanzisha katika msuruu huu wa matukio. Nilihisi ni kama jambo fulani lilikuwa likitendeka maishani mwangu ila sikujua ni nini. Nilikwenda Hollywood Blvd tena siku hiyo, sikuwa nikiwatafuta wale ndugu na dada kutoka kanisani, bali nilikuwa nikijaribu kuwakwepa. Badala yake nilikutana - bila kutarajia na mmoja wa wale dada wa kushuhudia pemberi mwa mtaa ambaye alinipa nakala ya injili na kunikaribisha kanisani jioni hiyo.

Nilimpa sababu isiyo na msingi, na kumwambia, "nitafikiria kuhusu jambo hilo" akanijibu kwa haraka, na kusema, "Ningefikiri sana kuhusu jambo hili, kwani inawezekana kwamba, huu ndio wakati wa mwisho ambao Mungu atajihuisha nawe!" Hamna kitu angeweza kusema ambacho kingenigusa zaidi ya maneno hayo. Wazo la Mungu kutojihusisha nami lilinigonga zaidi ya Kilo 1,000 za matofali usoni mwangu. Lilinisimamisha ghafla kwenye njia yangu. Nilikuwa kichaa, lakini sio kichaa kiasi cha kutotambua kwamba kuachwa na Mungu pekee yangu ndilo lingekuwa jambo la mwisho ambalo ningetaka maishani. Jambo hili liliogofya sana. Nilikuwa na uzuni nyingi tayari.

Nilitembea Hollywood Blvd, na kisha kwenye mitaa ya kando ambayo ilikuwa na majumba makubwa na viwanja (uga) pembezoni. Niliketi chini kwenye mo-

jawapo ya viwanja hivi na kungoja hadi wakati wa basi lilolokuwa likiwabeba watu kwenda kanisani ulipokaribia, kisha nikatembea kwenda mahali ambapo basi lilikuwa likiwabeba watu na kuchukua nafasi yangu mle ndani.

Safari hadi kanisani kule Saugus ilikuwa ndefu sana, lakini nilijihisi mwenye amani. Mmoja kati ya ndugu wa kikristo alitoa gita na kuwaongoza wote waliokuwa ndani ya basi kuimba nyimbo za injili hadi kanisani. Nilijihisi mwenye amani ingawaje haya yote yalioneckana mapya kwa wakati ule.

Tulipofika kanisani, wageni wote walioletwa na basi, walialikwa ndani na kuka kwa ibada. Sikuwahi kuingia kwenye kanisa la namna ile hapo awali, kanisa lilihisi kuchangamka. Halikuwa na ile hisia ya usu ndani yake ambayo makanisa mengine niliyokuwa nimehudhuria yalikuwa yamelowa. Ndugu na dada hawa wakati wa ibada waliimba nyimbo za injili kwa sauti kubwa. Walinua mikono yao hewani wakimsifu Bwana. Ilioneckana kana kwamba usiku huo kila mmoja kanisani humo alitoa ushuhuda wa namna fulani wa yale Mungu alikuwa ametenda maishani mwao. Baadhi yao walikuwa wamecumia madawa ya kulevyia kama mimi, baadhi hawakuwa wamecumia madawa. Baadhi walikuwa wamefungwa jela kisha kuachiliwa; baadhi walikuwa fukara wa mwisho na wengine waliojimudu kimaisha. Hawa walikuwa watu ambaao walikuwa kama mimi - wenye huzuni na wapotovu. Sasa walimkiri Kristo kama Mwokozi wao. Hawakuwa wamepotea tena, bali wamepatikana. Katika roho yangu, nilitaka kile walichowakilisha katika ibada usiku huo. Nilitaka uhai, lakini nilikuwa na tashwishi kuhusu mambo mengi. Shetani alikuwa akinitupia mamilioni ya tashwishi katika jaribio lake la mwisho la kuni-zuia kuokoka. Biblia inasema, "mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka." Wakati walimaita watu ambaao wangependa kuokoka usiku huo, Shetani alipoteza uwezo wake wa kunishikilia. Nilimwamini Bwana Yesu Kristo usiku huo nikwa nimepiga magoti mbele ya umati wote huo na nikaokoka! Mungu Asifiwe! Bwana asifiwe milele kwa uvumilivu na rehema aliyonionyesha! Nilikuwa nimezaliwa tena!

Usiku ule nilihisi Bwana akiingia ndani ya moyo wangu na sitakubali ka-

mwe jambo hili lipotee. Kwenda katika chumba cha maombi baada ya ibada huku nikijua bila tashwishi yoyote kwamba kweli kulikuwa na Mungu Mbinguni ambaye alinijali na kuyajibu maombi ndilo jambo la kutuliza zaidi nililowahi kujuwa. Bei ambayo Kristo alilipia haya ilikuwa damuke mwenyewe. Alikufa ili tuweze kuishi. Usiku huo alinileta mahali ambapo sitasahau daima. Alinipa ubatizo wa Roho Mtakatifu majuma mawili baada ya kuniokoa. Hakuna kitu kinachoweza kunithibitishia kwamba Mungu si wa kweli baada ya matukio haya yote. Yuko hai, na yu hai milele. Aliniokoa na anaweza kukuokoa. Nimeona maelfu ya watu wakiletwa kwa Yesu kupitia huduma hii tangu wakati huo. Nimeona watu wengi, wengi wakiponywa na nguvu za Mungu kutohana na magonjwa na maradhi waliyokuwa nayo. Nimeona maisha yaliyokuwa yameharibika kabisa (kama yangu) yakibadilishwa na kufanywa yenne kuzaa matunda. Siwezi kubadilisha maisha haya ya Ukristo na chochote ambacho dunia inanipa.

Tony na Susan Alamo ni watu waliotumiwa na Mungu kuwaleta maelfu ya watu wa tabaka mbali mbali kwa Kristo ili kupata maisha mapya ndani ya Kristo. Wote kwa pamoja walifanya hili bila ya uchoyo. Hawajawahi kumuomba mtu yeote malipo, ila tu tumtumikie Bwana. Susan alienda kuwa na Bwana mwaka wa 1982 na Tony ameendelea na injili kila siku tangu wakati huo. Angali anaendelea mbele. Mimi, na wengine wengi, tunatoa shukurani zetu kwao sio tu kwa kuwa na ari ya Mungu ndani yao ya kuwa na washuuda kwenye mitaa kila siku kuwafikia wengine wanaohitaji msaada, bali kwa kuwapa mahali ambapo watu kama mimi wangeweza kuishi maisha wakfu, ya kiungu na kujitenga na mambo ya ulimwengu huu mbaya. Bwana Asifiwe!

Kama unasoma ushuhuda huu na bado hujaokoka, usisubiri. Yesu Kristo ndiye kweli Mwokozi wa ulimwengu, na Anaweza kukupa kila kitu unachotamani. Aliniokoa, Alinipa kitu cha kupigia kelele, kitu cha kuishia na kufia. Anaweza kuktendea hayo hayo. Usisubiri. Mwambie aingie moyoni mwako leo!

Bwana Asifiwe,  
Steven Wedel

# JESHI NA JESHI LA ANGA LA MUNGU (WALINZI)

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 5)

moyo kufikia maisha ya milele.<sup>12</sup> Ni kwa ajili ya roho yako kuomba sala hii. Kisha ubatizwe, kwa kuzamishwa kabisa majini, kwa jina la BABA, la MWANA, na ROHO MTAKATIFU.<sup>13</sup> Soma toleo la Biblia la Mfalme Yakobo (KJV) la “THE BIBLE LEAGUE – Waenezaji wa Neno la Mungu tangu 1938];” na uzitimize amri.<sup>14</sup> Enenda katika ROHO wa MUNGU.<sup>15</sup>

**BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mweenye dhambi<sup>16</sup> ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.**<sup>17</sup> Ninaamini kwamba alikuwa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi zangu zote nilizozifanya hapo awali.<sup>18</sup> Ninaamini kwamba Mungu alimfufua YESU kutoka kwa wafu kupitia nguvu za ROHO MTAKATIFU<sup>19</sup> na ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikiliza maungamo ya dhambi zangu na maombi yangu haya.<sup>20</sup> **Ninafungua mlango wa moyo**

wangu na kukukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.<sup>21</sup> Nioshe dhambi zangu kwa damu uliyoimwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,<sup>22</sup> hutnikataa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yangu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia linasema hivyo.<sup>23</sup> NENO LAKO linasema hutamkataa ye yote na mimi nikiwemo.<sup>24</sup> Hivyo ninajua kwamba umenisikia, na ya kuwa umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.<sup>25</sup> Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuokoa roho yangu na nitaonyesha shukrani zangu kwa kufanya yale unayoniamuru na kwa kutotenda dhambi tena.<sup>26</sup>

Baada ya kuokoka YESU alisema ni lazima kubatizwa kwa kuzamishwa kabisa kwenye maji mengi kwa jina la BABA, MWANA na ROHO MTAKATIFU.<sup>27</sup> Kwa makini soma Biblia ya KJV, tafsiri ya Kiswahili ya The Bible League, Waenezaji wa Neno la Mungu tangu 1938 na ufanye inavyosema.<sup>28</sup>

BWANA anakutaka uwaambie wenye kuhusu wokovu wako. Unawezekusambaza makala ya Injili ya mchungaji Tony Alamo. Tutakutumia makala haya bila malipo. Tupigie simu ama

ututumie barua pepe kwa habari zaidi. Mshirikishe na mtu mwengine ujumbe huu.

Iwapo unataka dunia yote iokolewe, kama YESU anavyoamuru, basi usimwibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, “Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmeelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghali, ili kiwemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zilizookolewa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwe nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea ye ye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kundeza sana, asema Bwana wa majeshi” (Malaki 3:8-12).

**12** Muh. 3:19, Isa. 2:22 **13** Mat. 28:19-20 **14** 2 Tim. 2:15, 3:14-17 **15** Eze. 36:27, Rum. 8:1-14, Gal. 5:16-25 **16** Zab. 51:5; Rum. 3:10-12, 23 **17** Mat. 26:63-64, 27:54; Lk. 1:30-33; Yoh. 9:35-37; Rum. 1:3-4 **18** Mdo. 4:12; 20:28; Rum. 3:25; 1 Yoh. 1:7; Ufu. 5:9 **19** Zab. 16:9-10; Mat. 28:5-7; Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21; 10:17-18; 11:25; Mdo. 2:24, 3:15; Rum. 8:11; 1 Kor. 15:3-7 **20** Lk. 22:69; Mdo. 2:25-36; Ebr. 10:12-13 **21** 1 Kor. 3:16; Ufu. 3:20 **22** Efe. 2:13-22; Ebr. 9:22; 13:12, 20-21; 1 Yoh. 1:7; Ufu. 1:5, 7:14 **23** Mat. 26:28; Mdo. 2:21; 4:12; Efe. 1:7; Kol. 1:14 **24** Mat. 21:22; Yoh. 6:35, 37-40; Rum. 10:13 **25** Ebr. 11:6 **26** Yoh. 5:14, 8:11; Rum. 6:4; 1 Kor. 15:10; Ufu. 7:14; 22:14 **27** Mat. 28:18-20; Yoh. 3:5; Mdo. 2:38; 19:3-5 **28** Kumb. 4:29; 13:4; 26:16; Yos. 1:8; 22:5; 2 Tim. 2:15; 3:14-17; Yak. 1:22-25; Ufu. 3:18

**Tafadhali wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyingine ambavyo unaweza kuvutiwa navyo:**

**Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078**

**Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362**

**www.alamoministries.com • info@alamoministries.com**

**Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani amba wanataka kumtumikia BWANA kwa miyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.**

**Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.**

**Tafadhali wasiliana nasi kupitia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.**

**Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kiitwacho, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO**

**alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.**

**Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo Machapisho yetu na jumbe kwenye tebu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kupitia meli.**

**Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhali tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.**

**MAKALA HAYA YAMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)  
USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

**Kwa wale amba mko kwenye nchi nyingine, tunawashauri kutafsiri makala haya kwa lugha zenu. Iwapo mtachapisha tena, tafadhali jumuisha haki hii na usajili:**